



WAKALA YAONGOZA KATIKA UFUATILIAJI NA UZINGATIAJI WA MAADILI



Mkemia Mkuu wa Serikali, Profesa Samwel Manyele (wa pili kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi kutoka ofisi ya Rais Utumishi, Bw. Lambert Chialo (wa tatu kulia) na Bw. Rocky Setembo (wa tatu kushoto) pamoja na watendaji wa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali mara baada ya kukabidhiwa taarifa ya matokeo ya jumla ya ufuatiliaji na uzingatiaji wa maadili uliofanywa na Ofisi ya Rais ya Utumishi kwa kipindi cha miezi Sita (Julai – Disemba 2016).

Katika matokeo hayo Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeibuka ya kwanza kwa kupata asilimia 95 kati ya Taasisi za Umma 31 zilizofanyiwa tathmini.